Toleo na. 1

# TAMISEMI KAZINI

## Kishindo cha TAMISEMI 2021/22



**VIPAUMBELE:**

- Bil 322 kujenga barabara vijijini
- Ukamilishaji maboma ya Zahanati na Vituo vya afya
- Maboma ya madarasa nayo yaguswa
- Posho za madiwani

JUNI 2021

# YALIYOMO

UKURASA


1. Viongozi Wakuu ii
2. Tahariri 1
3. Kishindo cha OR - Tamisemi 2021/22 2
4. Bodi ya Wahariri 3
5. Vipaumbele 6 vya Mhe. Ummy 4
6. Siku 100 za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan 5
7. Miradi ya Kimkakati 7
8. Wakuu wa mikoa waaswa kusimami ukusanyaji wa mapato 8
9. Maelekezo kwa makatibu tawala wa mikoa 9
10. Silinde aagiza Maafisa Elimu Kata kusimamia miradi kwa weledi 11
11. Kamilisheni ujenzi wa Hospitali ya Wilaya – Dkt. Dugange 12
12. “Sijajiandaa kushindwa na sitegemei kushindwa” 13
13. Mhe. Ummy atoa maelekezo utekelezaji hoja za CAG 14
14. Maelekezo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan 15
15. Tengeni bajeti ya matengenezo ya magari - Mhe. Majaliwa 16
16. Miundombinu ya elimu 17
17. Halmashauri 4 kikaangoni, ukusanyaji mapato 19
18. Bilioni Tatu zanunua vifaa vya maabara 20
19. “Marufuku kutumia tiketi za bando” 21
20. Ziara ya Waziri wa Nchi OR - Tamisemi mikoani 22
21. Miundombinu ya afya 23
22. Mradi wa DMDP sasa kutekelezwa wilaya zote Mkoa wa Dar es salaam 24
23. Waziri Ummy aunda tume ya uchunguzi Soko la Kariakoo 25
24. Maelekezo ya jumla ya Waziri Ummy ziarani 26
25. Prof Shemdoe atengua kitendawili cha uhamisho 27
26. Wasichana wote wenye sifa wachaguliwa kujiunga na kidato cha tano, vyuo - 2021 28
27. Wakurugenzi acheni kubana fedha za lishe – Prof Shemdoe 29
28. Waziri Ummy na vikao vya idara 30
29. Waziri Ummy akoshwa na utendaji wa watumishi wa OR – Tamisemi 31
30. Serikali yaajiri watumishi 2,946 kwa kushirikiana na Mkapa Foundation 32
31. Prof. Shemdoe ataka tathmini ujenzi wa barabara za Mji wa Serikali 33
32. Wafanyakazi wa OR - Tamisemi waadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani 35
33. Mapokezi ya Katibu Mkuu OR- Tamisemi 36
34. Majaliwa aagiza somo la michezo kufundishwa kuanzia shule ya awali 37

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# Viongozi Wakuu



**Mhe. Ummy A. Mwalimu (Mb)**
Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI



**Mhe.David E. Silinde(Mb)**
Naibu Waziri OR- TAMISEMI



**Mhe. Dkt. Festo J. Dugange (Mb)**
Naibu Waziri OR- TAMISEMI



**Prof. Riziki S. Shemdoe**
Katibu Mkuu OR- TAMISEMI



**Dkt. Grace E. Magembe**
Naibu Katibu Mkuu (AFYA)



**Gerald G. Mweli**
Naibu Katibu Mkuu (ELIMU)



# TAHARIRI

TUNAPOTOA toleo la kwanza la Jaridanla TAMISEMI KAZINI tangu uongozi wa Awamu ya Sita uingie madarakani sambamba na uongozi mpya wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninapenda kuwashukuru sana Viongozi waliopita yaani Mhe. Selemani S.Jafo aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja naaliyekuwa Katibu Mkuu Eng. Joseph Nyamhanga. Hakika walifanya kazi kubwa na sisi sasa tutaendelea pale walipoishia.

Katika kuendeleza kazi ile nzuri iliyoanzishwa na watangulizi wetu, tutafakari kauli hii, "TAMISEMI, sio Ngumu bali ni Kubwa." Kauli hii ilitolewa na Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu, katika siku yake ya kwanza alipowasili ofisini ikiwa ni baada ya kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, kutumikia ofisi hii. Kutokana na kauli ya kiongozi wetu ndani ya Wizara, kila mmoja wetu kuanzia ngazi ya Wizara, Mikoa, Halmashauri, tunapaswa kujitafakari kwa namna gani Waziri kuonesha njia, ili kuleta tija iliyo kusudiwa.

Umoja wetu, ushirikiano na kujitoa kwetu ni nguzo muhimu kwa sababu ya jukumu tulilonalo la kujenga taasisi inayojiamini na iliyo tayari kushiriki kuleta maendeleo.

Tangu akabidhiwa kijiti cha kuongoza wizara, shauku yake ilikuwa kuona tunasonga mbele, na hapo tulijiwekea vipaumbele ambavyo kila mmoja wetu kwa nafasi yake, anapaswa kuvitekeleza kulingana na nafasi yake. Mfano, kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa Mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuziwesha Halmashauri kujitegemea kimapato na kutatua changamoto za wananchi hususani katika sekta ya Afya, Elimu na Miundombinu na kuziba mianya ya upotevu wa mapato katika Halmashauri, mathalani tulitia msisitizo kwenye nidhamu kwa watumishi katika ukusanyaji wa mapato na kutoa huduma bora kwa wananchi katika ngazi zote.

Kwa kipindi cha miezi mitatu cha uongozi mpya wa TAMISEMI, yapo mambo kadhaa ambayo tumefanikiwa kwa namna moja au nyingine, lakini lazima tujiulize, tumekidhi haja na kiu ya Watanzania tunaowahudumia? Kwa kipindi hiki cha kuanzia Aprili – Juni 30 mwaka huu, tumepeleka takribani shilingi bilioni 74 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya pamoja na Vifaa Tiba na Vitendanishi kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma.

Katika Sekta ya Elimu tumeweza kupeleka takribani shilingi bilioni 260 kwa ajili ukamilishaji na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule za msingi na sekondari, vyumba vya maabara, mabweni na kugharamia Elimu bila ada. Kwenye eneo la miundombinu, uongozi umeweza kupeleka jumla ya shilingi bilioni 37.6 ambazo zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa barabara kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya kilometa 3,357.14, na kurekebisha maeneo korofi kilometa 1,411.34 na kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara kilometa 1,033.16. Tumefanikiwa kupata kibali na kutangaza ajira 6,949 za walimu, na ajira 2,726 katika sekta ya afya, ambapo Watanzania wenye sifa wamefaniki imeundwa na Watanzania wenyewe. Kupitia tahariri hii sintoweza kueleza yale yote ambayo Ofisi ya Rais-TAMISEMI tumetekeleza kwa kipindi cha miezi mitatu, lakini itoshe kusema kupitia Jarida letu la TAMISEMI Kazini, wataalamu wetu wameandika mengi yaliyofanyika na kila mmoja anaweza kusoma na kujua kazi mbalimbali zilizofanyika.

Rai yangu ni kuwahimiza watumishi wote wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuendelea kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa na kuzingatia weledi huku wakitanguliza uzalendo na maslahi mapana ya Taifa mbele.

Karibuni TAMISEMI ya Wananchi, Hatupoi, Kazi Iendelee.

Asanteni

Prof. Riziki S. Shemdoe
KATIBU MKUU

# Kishindo cha OR - TAMISEMI 2021/2022







Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), imeipitishiwa na Bunge Makadirio ya Mapato na Matumizi kiasi cha Sh 7,683,329,644,800 yenye vipaumbele sita.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mhe.Ummy Mwalimu amesema bajeti hiyo inajumuisha Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu, Fungu Na. 2 na mafungu 26 ya mikoa yanayojumuisha halmashauri 184.

Amesema katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kuzingatia vipaumbele utoaji wa huduma bora za afya ya msingi ikijumuisha ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba pamoja na ujenzi wa miundombinu ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri.inu

Pia amesema utoaji wa huduma bora za elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kununua vitabu, vifaa vya maabara pamoja na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara, nyumba za walimu, shule za sekondari za sayansi za wasichana, ujenzi wa shule za kutwa za kata pamoja na utengenezaji wa madawati kwa shule za msingi.
Vingine ni ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini, kuwawezesha wananchi kiuchumi; kuimarisha utawala bora na usimamizi wa rasilimali na kujenga mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji wa viwanda mijini na vijijini.

Maeneo muhimu yaliyoguswa kwenye bajeti hiyo ni ulipaji posho za mwezi za madiwani kwa halmashauri 168, posho ya mafuta ya 100,000 kila mwezi kwa watendaji wa kata na Maafisa Tarafa nchi nzima, Sh bilioni 320 kujenga barabara bora za vijijini kupitia TARURA(barabara bora kila kijiji) na kukamilisha maboma ya zahanati.

# SERIKALI YAMWAGA AJIRA KADA ZA AFYA NA ELIMU

SERIKALI imeajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya 2,726 kwa ajili ya hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati na walimu 6,949 wa shule za msingi na sekondari watakaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Wahitimu kutoka kwenye vyuo vya elimu ya juu, vyuo vya ualimu na vyuo vya afya vinavyotambuliwa na Serikali walitangaziwa kutuma maombi yao ya nafasi za kazi kuanzia tarehe 09 - 23 Mei, 2021.

Baada ya tangazo hilo, waombaji wa kada ya ualimu walikuwa 99,583 na wataalamu wa kada ya afya walikuwa 37.437 wakiwemo wenye ulemavu 1,099 waliomba nafasi hizo.

Aidha, baada ya kukamilisha taratibu zote za uchakataji wa maombi walimu 6,949, ambapo 3,949 ni wa shule za msingi na 3000 wa shule za sekondari, na wataalam wa kada za afya 2,726 wamepangiwa vituo vya kazi.

MFUKO WA AFYA WA JAMII
CHF Iliyoboreshwa
TUMEJIPANGA
JIUNGE TUKUHUDUMIE

# BODI YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**
Prof.Riziki Shemdoe
Katibu Mkuu
Ofisi ya Rais - TAMISEMI

**MHARIRI**
Nteghenjwa Hosseah
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
Angela Msimbira
Methew Kwembe
Fred Kibano
Atley Kuni
Asila Twaha
Rafael Kilapilo

**MSANIFU KURASA**
Godfrey Isinika

JARIDA LA TAMISEMI KAZINI
LIMEANDALIWA NA
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
MJI WA SERIKALI – MTUMBA
MTAA WA TAMISEMI
S.L.P 1923
ps@tamisemi.go.tz

# VIPAUMBELE 6 VYA MHE. UMMY



*"Kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa Mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuziwesha Halmashauri kujitegemea kimapato na kutatua changamoto za wananchi hususani katika sekta ya Afya, Elimu na Miundombinu"*

*"Kuboresha miundombinu ya barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Wakala wa barabara za vijijini na Mijini (TARURA) pamoja na miundombinu mingine"*

*"Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora kwa Mwananchi"*

*"Kuwezesha Wananchi Kiuchumi hususani ni Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ikiwemo kukusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa ili wananchi wengi wanufaike"*

*"Kudhibiti matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo zinazopokelewa kwenye Halmashauri"*

*"Kuziba mianya ya upotevu wa mapato katika Halmashauri"*



# SIKU 100 ZA MHE. RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetaja mafanikio yaliyopatikana katika maeneo manne ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ikiwamo mabilioni ya fedha yaliyopelekwa kuimarisha huduma za afya msingi kwa wananchi.

Akizungumzia mafanikio hayo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Ummy Mwalimu (Mb), amesema tangu Rais Samia aapishwe Machi 19, mwaka 2021, Ofisi hiyo imepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake ya kusimamia shughuli za maendeleo na utawala bora katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alitaja maeneo hayo yaliyopata mafanikio kuwa ni Huduma za AfyaMsingi, Sekta ya Elimu Msingi na Sekondari, Miundombinu ya Barabara, Utawala na Usimamizi wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri.

Upelekaji wa Huduma za AfyaMsingi kwa wananchi

Akizungumzia eneo hilo, anasema kwa kipindi cha siku 100, Serikali imepeleka kwenye halmashauri 34 kiasi cha Sh bilioni 20.3 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri ambapo ujenzi unaendelea.

Aidha, anasema halmashauri 76 zimelekewa fedha kiasi cha Sh bilioni 11 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu kila halmashauri.

Vilevile, anasema kupitia mradi wa matokeo ya ufanisi (Result Based Financing -RBF) umefanyika uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya ambapo zahanati 279, vituo vya afya 46 na hospitali 22 za wilaya zimepatiwa fedha kiasi cha Sh bilioni 30.8 ili kuviwezesha vituo hivyo kufika ngazi ya nyota tatu katika ubora wa utoaji huduma.

" Kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya kiasi cha shilingi bilioni 1.6 zimetolewa kwa ajili ya kununua vifaa tiba vya usingizi katika vituo vya afya 32 ili kuviwezesha vituo hivi kufanya upasuaji ikiwemo upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni. Kupitia Mradi wa Commodity Import Support, Serikali imewezesha ujenzi wa vituo vya afya 20 katika halmashauri 20 na kila kituo cha afya kimepatiwa kiasi cha shilingi milioni 500,"anasema.

Alibainisha kuwa lengo la ujenzi wa vituo vya afya ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ili kupunguza vifo hususani vinavyotokana na uzazi.

"Pia, Serikali katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya, ndani ya siku 100 za Rais Samia, Serikali imeajiri watumishi 2,726 wa afya wakiwemo madaktari, wauguzi na watalamu wa maabara na kuwasambaza katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri," anasema.

Usimamizi wa Elimu Msingi na Sekondari

inaendelea uk. 6

*inatokaa uk. 5*



Katika usimamizi wa elimu ndani ya siku 100 za Rais Samia, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ambapo Sh.bilioni 152.1 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi na sekondari huku kiasi cha Sh bilioni 17.5 zimetolewa na kupokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya maabara 582 za sayansi katika halmashauri mbalimbali nchini.

Pia alisema Sh bilioni 8.8 kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 110 kwa baadhi ya shule za sekondari zenye changamoto ya wanafunzi kutembea umbali mrefu.

" Serikali pia imeendelea kuongeza wigo wa wanafunzi waliofaulu kutoka kidato cha nne kwenda kidato cha tano ambapo katika kipindi hiki wanafunzi 87,663 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (kati ya hao wasichana ni 41,885 na wavulana ni 45,778 sawa na ongezeko la wanafunzi 14,562 ikilinganishwa na wanafunzi 73,101 waliochaguliwa mwaka 2020,"anasema.

Hata hivyo, anasema katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, wanafunzi wote wasichana waliokidhi vigezo wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya kati.

" Katika kutekeleza azma ya kuwapatia wanafunzi elimumsingi bila ada, Serikali imetoa Sh bilioni 83.2 ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia. Katika kuboresha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi, Serikali imeajiri walimu 6,946 wa shule za msingi na sekondari na kufanya msawazo wa walimu wa shule za msingi na sekondari kwa halmashauri zote 184,"anasema.

Kuhusu upandishaji wa madaraja, anasema ndani ya muda huo walimu 119,887 waliotimiza vigezo walipandishwa madaraja kati ya 122,574 waliokasimiwa sawa na asilimia 97.8 na walimu 622 walisajiliwa na kupatiwa namba ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Miundombinu ya barabara

Anasema kwa muda huo, Sh bilioni 37.6 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya kilometa 3,357.14, kurekebisha sehemu korofi kilometa 1,411.34, kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara kilometa 1,033.16.

Usimamizi wa mapato ya ndani ya halmashauri

Anasema halmashauri zimeendelea kukusanya mapato ya ndani kutokana na vyanzo mbalimbali ambapo zaidi ya Sh bilioni 178.945 zimekusanywa katika kipindi hiki na kati ya fedha hizo Sh bilioni 15.615 zimetolewa mikopo kwa vikundi 3,757 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

" Katika utekelezaji wa mkakati wa usimamizi wa mapato ya halmashauri, umefanyika ufungaji wa mifumo ya TEHAMA katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam kwa kiasi cha shilingi bilioni 236.459,"anasema.

Anazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuendelea kupeleka maendeleo kwa wananchi na kuwashirikisha katika maamuzi yanayohusu maendeleo yao.

# MIRADI YA KIMKAKATI



*Soko la Kisutu - Jijini Dar es Salaam*



*Soko la Chifu Kingalu - Manispaa ya Morogoro*

# WAKUU WA MIKOA WAASWA KUSIMAMIA UKUSANYAJI MAPATO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(OR-TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) amewataka wakuu wa mikoa kuwa waangalifu na suala zima la ukusanyaji wa mapato na kuwatahadharisha juu ya ujanja mwingi unaofanywa na viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji mapato.



*Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu akizungumza na wakuu wa mikoa mara baada ya kuapishwa.*

Mhe. Ummy ameyasema alipokuwa akizungumza na wakuu wa mikoa katika Ofisi ndogo za OR -TAMISEMI zilizopo Dar es Salaam muda mfupi baada ya kuapishwa. Amesema kuwa kumekuwa na upotevu mkubwa wa mapato katika baadhi ya halmshauri kutokana na wengi wao kutopenda kutumia mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa fedha ambayo kwa kiasi kikubwa imeongeza udhibiti.

"Halmashauri nyingi wamekuwa wajanja wakidai makusanyo ni hafifu lakini ukiwabananunaziona fedha zipo. Niwaambie tu ukitaka kugombana na mtumishi wa halmashauri wewe mtoe kwenye ukusanyaji, wanang'ang'ania na mpaka walimu nao unawakuta wanakusanya mapato na kuacha taaluma zao, nendeni mkasimamie,"amesema Ummy.

Mhe. Ummy ameeleza kuwa halmashauri nyingi zimekuwa hazitumii mifumo ya kielektroniki na badala yake zinatumia fedha mbichi jambo linalosababisha upotevu wa mapato.

"Nawataka mkahakikishe fedha hizo zinakusanywa kikamilifu ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika utatuzi wa kero mbalimbali za wananchi hasa katika sekta ya elimu na afya ambapo ndipo panatajwa kuwa na changamoto nyingi zinazohitaji utatuzi," amesema.

Pia Mhe. Ummy amesema hatua ya wao kuwasaidia wananchi utatuzi wa kero mbalimbali wanazokabiliana nazo ni jambo jema pia ni sehemu ya sadaka na baraka kwa mwenyezi Mungu hivyo ni vyema kwa nafasi zao waende wakawabane wakurugenzi dhidi ya makusanyo hayo ya mapato ili yaweze kusaidia utatuzi wa kero hizo.

"Naomba twende tukamsaidie Rais kusimamia halmashauri zetu na tukajipange na madarasa kwa ajili ya mwaka 2022 kwa sababu tunakabiliwa na uhaba wa maadawati zaidi ya milioni moja, mashimo ya vyoo pamoja na nyumba za walimu. Hakikisheni katika kila bajeti zenu walau mnajenjenga nyumba za walimu pamoja na kuongeza madarasa, na mzisimamie sekretarieti za mikoa ili ziweze kutimiza wajibu wao," amesema.

Aidha ameongeza kuwa Ofisi yake itawakuwa wazi kwa wakuu wa mikoa hao kuhusu fedha zote zitakazotumwa katika mikoa ili kuondoa vificho vinavyokuwepo katika ofisi za wakurugenzi pamoja na makatibu tawala kwa lengo la kuwasaidia kuwabana pale ambapo kutakuwa na kificho kutoka kwa watendaji hao wa ofisi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Tellack amesema wamejipanga kikamilifu kwenda kutimiza majukumu yao na zaidi suala zima la ukusanyaji wa mapato ambayo ndiyo kiini cha maendeleo ya nchi.

" Nipende kukuhakikishia Mheshimiwa Waziri kuwa tutaenda kusimamia ukusanyaji mapato, pamoja na kutekeleza majukumu yetu kikamilifu ili kumsaidia Rais, uwezo huo tunao na hatutakuangusha,"amesema Mhe. Tellack.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. David Kafulila mbali na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini katika nafasi hiyo, amesema anakwenda kutekeleza masuala yote ambayo ni kipaumbele kwa Serikali ikiwemi afya, elimu na ukusanyaji wa mapato.

# MAELEKEZO KWA MAKATIBU TAWALA WA MIKOA


*Mhe. Ummy Mwalimu(Mb) (Waziri wa Nchi, OR - TAMISEMI)*

1.Sekretarieti ya Mkoa ina wajibu wa kuzisimamia, kuzishauri na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza na kutimiza majumumu yake mkalisimamie hilo.

2.Tutaziimarisha Sekretarieti za Mikoa kwa kuhakikisha kuwa watumishi wa ngazi hiyo wanauwezo mkubwa katika kushauri na kutoa mchango wa kuleta maendeleo katika Mamlaka za Sekretarieti

3.Tutatenga fedha kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ili Sekretarieti za Mkoa ziweze kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

4 Kasimamieni ukusanyaji wa Mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

6.Wekeni Mkakati wa kuhakikisha tunafikia lengo la ukusanyaji wa mapato tulilojipangia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

7.Simamieni Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinatenga fedha za mapato kwa ajili ya kuelekeza kwenye miradi ya maendeleo inayotatua changamoto za wananchi ikiwemo elimu, afya na miundombinu ya barabara.

8.Simamieni matumizi ya fedha za mapato ya ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

9.Hakikisheni matumizi sahihi ya fedha za miradi ya maendeleo zinazotoka Serikali Kuu.

10.Ongezeni usimamizi na ufuatiliaji kwenye miradi inayotekelezwa kwa 'Force Account' ili kuhakikisha miradi hiyo inajengwa kwenye ubora uliokusudiwa.

Mhe. Ummy Mwalimu(Mb)
Waziri wa Nchi, OR - TAMISEMI
2 Juni 2021

1. Simamieni nidhamu ya watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kwa kuwa nyie ndio wakuu wa Utumishi katika Mikoa chukueni hatua kwa wale ambao nidhamu zao haziridhishi.

2. Sisitizeni wakurugenzi wa halmashauri kutokukwepa majukumu yao kwa kuwa Mamlaka za watumishi wengi zipo ndani ya uwezo wao kila mtu atimize majukumu yake

3. Simamieni Sheria, Taratibu na Kanuni lakini busara pia itumike katika kutoa maamuzi

4. Fanyeni kazi kwa ushirikiano na watumishi walioko chini yenu, kila mmoja akitimiza majukumu yake kwa weledi tutafanikiwa kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi

6.Hakikisheni mnawasimamia watumishi wanaoshughulikia masuala ya uhamisho kwa umakini mkubwa ili wasichafue taswira ya halmashauri, mikoa na wizara.

7. Tatueni kero za wananchi kwa kuwa wao ndio waliotupatia dhamana ya hii, wasikilizeni na kutatua changamoto zao.

8. Simamieni ukusanyaji wa mapato katika halmashauri zenu elekezeni nguvu kwenye chanzo cha ushuru wa huduma hasa kwenye vituo vya mafuta vilivyoko katika halmashauri

Prof. Riziki Shemdoe
Katibu Mkuu, OR - TAMISEMI
2 Juni 2021


*Waziri wa Nchi, OR - TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu (katikati) akiwa na makatibu tawala wa mikoa*

# MAELEKEZO KWA MAKATIBU TAWALA WA MIKOA



*Gerald Mweli*
*Naibu Katibu Mkuu (Elimu)*

1.Kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Mradi mpya wa Elimu Sekondari (Sequip) na tunaanza na ujenzi wa shule za sekondari za wasichana 26 kwa kila mkoa kwa pamoja mkubaliane sehemu sahihi ya kujenga shule hiyo.

2. Kupitia mradi huo pia (Sequip) tutajenga shule mpya 1000 kwa sasa tuna kata 719 ambazo hazina shule hivyo tutajenga kwenye kata hizi na zile ambazo zina shule lakini zina wanafunzi wengi.

3. Kusimamia kikamilifu ujenzi wa madarasa ya kuwapokea wanafunzi cha kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2022 tusisubiri zimamoto na tayari tumeshatoa makisio.

4. Tukasimamie ukusanyaji wa takwimu sahihi za elimu ili zitusaidie kufanya maamuzi na kupeleka rasilimali ni aibu kuona shule ya matope kwenye vyombo vya habari wakati tuna maafisa elimu kata wanaotakiwa kutoa taarifa hizi.

5. Tuzisimamie halmashauri katika kuhakikisha kwamba wanaandaa mazingira wezeshi kwa walimu wa ajira mpya watakaoajiriwa hivi karibuni.

6. Kusimamia mfumo wa uhamisho wa walimu utakaoanza kufanya kazi Julai mwaka 2021.

7. Kuhamasisha wananchi kutumia namba za kituo cha huduma kwa wateja kuwasilisha kero zao. Tumeelekeza kila ofisi ya serikali ibandikwe namba ya kituo hiki.

Gerald Mweli
Naibu Katibu Mkuu (Elimu)
2 Juni 2021



*Dkt. Grace Magembe*
*Naibu Katibu Mkuu (Afya)*

1. Udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, RS na CMT wote wajengewa uwezo ili wafanye ukaguzi wa bidhaa za afya kila robo.

2. Taarifa ya vizazi na vifo vitokanavyo na uzazi ni lazima viwasilishwe kwenye vikao vya menejimenti vya mkoa na halmashauri.

3. Kusimamia upatikanaji wa huduma bora katika vituo vya kutolea huduma.

4. Kuwasimamia wakurugenzi wa halmashauri kuwapa posho za kujikimu watumishi wapya wa afya watakaoajiriwa hivi karibuni wakati wanasubiri kuingizwa kwenye utaratibu wa malipo Serikalini.

5. Kusimamia kikamilifu moundombinu ya afya inayoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali nchi nzima.

Dkt. Grace Magembe
Naibu Katibu Mkuu (Afya)
2 Juni 2021

# SILINDE AAGIZA MAAFISA ELIMU KATA KUSIMAMIA MIRADI KWA WELEDI



NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), David Silinde, (pichani) amewaagiza Maafisa Elimu Kata nchini kusimamia rasilimali fedha za miradi ili kuongeza tija kwenye sekta hiyo muhimu hapa nchini.

Akifungua kikao kazi kilichowakutanisha Maafisa Elimu Kata Tanzania Bara ambao agenda kuu ni kuunda umoja wao wa Waratibu Elimu Kata Tanzania Bara (UMEKTA) Jijini Dodoma, Silinde amesema miradi mingi kwenye sekta ya elimu haikamiliki kwa wakati na hivyo jamii inayoizunguka miradi hiyo kuchelewa kupata manufaa ya miradi hivyo hakuna budi Waratibu Elimu Kata wahusishwe moja kwa moja na kwamba baadhi yao wanazembea na kuisababishia Serikali hasara.

“Kuhusu usimamizi wa fedha na miradi ya elimu, kila afisa elimu Kata asimamie miradi na fedha zote za Serikali ndani ya kata yake kwa shule zote za msingi na sekondari,” anasema Silinde.

Aidha, Silinde amesema hali ya uandikishwaji imeongezeka na hili ni kutokana na Serikali kutoa Elimu Bila Malipo hivyo kuwataka Maafisa hao kuwajibika katika kusimamia elimu katika maeneo yao.

Kuhusu taaluma amewataka kuhakikisha wanasimamia kikamilifu suala la elimu ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi nchini kwenye shule za msingi na sekondari akiwaasa baadhi ya Maafisa Elimu Kata kutowajibiki katika usimamizi wa shule za sekondari katika maeneo yao na kusababisha kutokuwa na taarifa muhimu za kielimu lakini pia watakaowakwamisha kusimamia elimu ya sekondari watolewe taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe.

Pia amewataka viongozi hao kulisimamia suala la ufundishaji na ujifunzaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) na elimu ya awali linakuwa kipaumbele kwao kwa kuhakikisha wanalisimamia ili kujua changamoto zinazowakabili wanafunzi.

Kwa upande wake, Gerald Mweli ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI (ELIMU), ametoa rai kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kuwajengea uwezo na kuwaamini maafisa hao katika eneo la rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao ikiwa ni pamoja na rasilimali fedha na pia amewataka maafisa hao kutunza pikipiki walizopatiwa na Serikali kwa lengo la kukagua taaluma kwenye maeneo yao na kuipaisha sekta ya elimu nchini.

Mweli amesema pia shule za msingi zimeongezeka kutoka 16,899 waka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020 na shule za sekondari kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi 5,330 mwaka 2020 wakati vyumba vya madasa kwenye shule za msingi kutoka 115,665 mwaka 2015 hadi 136,292 mwaka 2020.

Naye, Robert Tesha ambaye ni Mwenyekiti wa Waratibu Elimu Kata Mkoa wa Dodoma kwa niaba ya washiriki wote ameahidi kutimiza wajibu wao ili kuinua kiwango cha taaluma nchini pia watajadili mambo muhimu yanayohusu katiba kwa muda wa siku mbili yatakayosaidia umoja huo uanze kufanya kazi mara moja.

Akitoa neno la shukrani, Paul Kamele Mwenyekiti wa Waratibu Elimu Kata Mkoa wa Morogoro amesema jukwaa la maafisa hao lilikuwa liwe limeanza kwa muda mrefu ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

# KAMILISHENI UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA – DKT. DUGANGE



*Muonekano wa majengo yanayoendelea kujengwa katika Hospitali ya Wilaya ya Gairo)*

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Dkt. Festo Dugange amewaagiza viongozi wakuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo kuhakikisha wanasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi ya maendeleo wilayani humo na ikamilike kwa muda uliopangwa.

Dkt.Dugange ametoa agizo hilo wakati alipokutana na viongozi wa wilaya, watendaji wa halmashauri pamoja na watumishi wa Idara ya Afya wakati akikagua ujenzi wa majengo saba ya Hospitali ya Wilaya ya Gairo na ujenzi wa boma kwenye zahanati ya Mogohigwa iliyopo Kata ya Chigela.

“Nakuagiza Mkurugenzi ukishirikiana na Mwenyekiti wa Halmashauri, hebu kasimamieni kwa ukaribu miradi yote na mhakikishe inakamilika kwa wakati ili wananchi waanze kunufaika na huduma tulizo kusudia hususani kwa hii miradi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na zahanati mpya ya Mogohigwa, lakini pia hata kwa miradi ya urekebishaji miundo mbinu kwenye zahanati za zamani,” amesema.

Amefafanua kuwa ni lazima kuwepo na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha zinazotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya kupitia miradi ya ujenzi wa hospitali za wilaya, uboreshaji wa miundombinu kwenye kituo cha afya na zahanati pamoja na ujenzi wa zahanati mpya ili thamani ya pesa ilingane na ubora wa majengo yaliyopo na miundo mbinu mingine.



*Naibu Waziri, Dkt. Festo Dugange akikagua maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Gairo*

“ Mkurugenzi hili nalo ni muhimu sana kulizingatia, Serikali inaleta fedha nyingi kwa ajili ya sekta ya afya, lengo ni kuhakikisha wananchi wake wananufaika na ubora wa huduma, hivyo thamani na ubora wa majengo pamoja na miundo mbinu yake lazima ilingane kabisa na thamani ya fedha zilizotumika,” amesisitiza Naibu Waziri.

Aidha Dkt. Dugange amemwagiza Halmashauri hiyo kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuhakikisha wanafikia lengo la asilimia 100 katika mwaka wa fedha 2021/2022.

“Suala la makusanyo kwa Gairo bado mpo chini sana ni asilimia 67 tu ya lengo, naagiza pia lipewe uzito zaidi ili kufikia lengo la kukusanya kwa asilimia 100. Kupitia makusanyo ya ndani mtakuwa na nguvu ya kujiendesha bila kuwa na utegemezi kutoka Serikali kuu, pia itasaidia kuimarisha miundombinu katika utoaji hudumwa kwa jamii,” amesema.



*Naibu Waziri, Dkt. Festo Dugange akisalimiana na wagonjwa waliofika kupata huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Mvomero, wakati wa ziara yake mkoani Morogoro*

# "SIJAJIANDAA KUSHINDWA NA SITEGEMEI KUSHINDWA"




*Mhe Ummy Mwalimu*
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tamisemi*
*Mapokezi ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu (Afya)*
*08 April 2021*

1 Sijajiandaa kushindwa na sitegemei kushindwa kuongoza kwa mafanikio Ofisi ya Rais TAMISEMI.

2 Sitaki kuona mtoto wa kitanzania anasomea chini ya mti au anakaa chini kwakukosa dawati, tuna wajibu wa kujenga vyumba vya madarasa, maabara, nyumba za walimu pamoja na kuweka madawati ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

3 Tutoe muongozo wa uhamisho kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili watumishi wasihangaike na suala hili la uhamisho.

4. Tutatue kero za walimu hususan posho za kujikimu kwa walimu wa ajira mpya na stahiki zingine kwa walimu wna watumishi wote.

5. Ndani ya siku 100 mchakato uanze kwa kuanzisha Idara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## MAELEKEZO YA KIUTEKELEZAJI – HOJA ZA CAG

1 Katika kuhakikisha kuwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaongeza uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kuzisimamia halmashauri, ninakusudia kuandaa na kusaini Mikataba ya Ufanisi (Performance Contract) kati yangu na Wakuu wa Mikoa wote nchini.

2 Halmashauri zilizopata Hati Mbaya na Hati eenye Shaka ziwabainishe wataalam wa fedha wenye CPA (T) ambao walisaini taarifa za hesabu za mwisho kuthibitisha kwamba taarifa hizo ni sahihi na hazina makosa ilihali Ukaguzi wa CAG umebainisha kuwa taarifa hizo hazikufuata viwango wa kimataifa wa ukaguzi wa mahesabu na wafikishwe kwenye Bodi ya Wahasibu (NBAA) na wachukuliwe hatua kwa mujibu wa taaluma zao.

3 Wataalamu wa fedha wenye CPA (T) wanaotakiwa kufikishwa kwenye Bodi ya Wahasibu(NBAA) ili wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa taaluma zao ni waleambao halmashauri zao zimepata Hati Mbaya na Hati zenye Shaka na wao kama wataalamu walisaini taarifa ya hesabu za mwisho kuthibitisha kwamba taarifa hizo ni sahihi na hazina makosa ilihali Ukaguzi wa CAG umebainisha kuwa taarifa hizo hazikufuata viwango wa kimataifa vya uandaaji wa hesabu za mwisho.

# Mhe. Ummy atoa maelekezo ya kiutekelezaji - hoja za CAG

## WAKUU WA MIKOA

*"Hoja nyingi zilizotajwa na CAG zinatokana na baadhi ya Watumishi wa Halmashauri kutowajibika ipasavyo au kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu; Hivyo, Wakuu wa Mikoa yote wahakikishe kuwa Sekretarieti za Mikoa zinatekeleza majukumu yao ya kisheria kwa ukamilifu ikiwemo kuzisimamia kwa karibu Halmashauri"*

## WAWEKA HAZINA

*"Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Nidhamu zihakikishe kuwa hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya Waweka Hazina waliohusika na uandaaji wa taarifa za hesabu za mwisho katika Halmashauri nane (8) zilizopata Hati Mbaya na Halmashauri 53 zilizopata Hati Zenye Shaka.*

*Waweka Hazina hao hawakutekeleza kikamilifu wajibu wao wa kutunza kumbukumbu za fedha na kuandaa taarifa sahihi. Hii ni kinyume na Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 Agizo la 27(3)"*

## WAKURUGENZI

*"Kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 na Agizo la 31(1) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa – 2009, Wakurugenzi wa Halmashauri wana wajibu wa kuhakikisha kuwa taarifa za hesabu za mwisho zinaandaliwa kwa usahihi.*

*Hivyo, nimeishauri Mamlaka ya Nidhamu ya Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo hazikufanya vizuri katika ukaguzi huu iwachukulie hatua stahiki kadiri ya itakavyoona inafaa"*

## WAKUU WA VITENGO VYA NDANI

*"Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Nidhamu zihakikishe kuwa hatua stahiki zinachukuliwa kwa Wakuu wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani wa Halmashauri 54 ambao hawakukagua taarifa za hesabu za mwisho kabla ya kuziwasilisha kwa CAG"*

## WATUMISHI

*"Aidha, Watumishi wote wa Halmashauri ambao hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo au kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu wabainishwe na kuchukuliwa hatua stahiki za kisheria na kinidhamu"*

# MAELEKEZO YA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN



1 Kero zote za Wananchi zitatuliwe katika ngazi ya msingi, labda zile za kitaifa tu ndio ziletwe kwetu, vinginevyo Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi watawajibishwa kwa kushindwa kutatua kero za wananchi.

2 Kwa upande wa elimu, shule ishirini na sita (26) za wasichana nchi nzima zianze kujengwa mara moja kwa sababu ina bajeti yake ipo hivyo utekelezaji uanze mara moja.

3 Kuna nafasi za ajira takribani 6,000 katika Kada ya Ualimu ambazo ziko wazi kwa sababu mbalimbali kama vile kustaafu, kufariki na kuacha kazi, hizi ni tofauti na ajira mpya: TAMISEMI kwa kushirikiana na utumishi nafasi hizo zijazwe mara moja.

4 Upande wa afya, hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati zimeendelea kujengwa na hivi sasa zinahitaji zaidi vifaa tiba na wataalamu wa afya kwa sasa tupeleke vifaa hivyo na ajira za afya zitolewe ili wataalamu katika vituo hivyo wapatikane wa kutosha.

5 TARURA tumewapa kazi ya ujenzi wa barabara za vijijini na mijini lakini kuna maeneo mengi bado barabara zake ni mbovu sana kutoka na uwezo mdogo wa kifedha wa TARURA: sasa kwa halmashauri zenye mapato ya kutosha zitumie mapato hayo ya ndani kutatua changamoto ya ubovu wa miundombinu ya barabara.

6 Halmashauri zote zikusanye mapato ya ndani kikamilifu na matumizi yake yazingatia sheria zilizowekwa za matumizi ya fedha za umma.

***Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***akiwaapisha Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Idara za Serikali.***

***IKULU DAR ES SALAAM, APRIL 6,2021.***

# TENGENI BAJETI YA MATENGENEZO YA MAGARI - MHE. MAJALIWA

WAZIRI Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha wanapanga bajeti ya kufanyia matengenezo magari ya halmashauri ili yadumu kwa muda mrefu.

Mhe.Majaliwa ametoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na Maafisa Elimu wa halmashauri ya zote 184 nchini kwenye uzinduzi wa zoezi la ugawaji wa magari kwa maafisa hao yaliyonunuliwa kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo(EP4R), lililofanyika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya Kibasila Mkoani Dar-es-salaam.

"Kuna baadhi ya halmashauri hazitengi bajeti kwa ajili ya matengenezo ya magari yao, na kusababisha magari hayo kuharibika mapema na kuwekwa gereji bila matengenezo ya halmashauri zao."

"Maafisa elimu wa wilaya mkikabidhiwa magari haya leo na tukalikuta gari limekaa na halifanyi kazi kwa kukosa matengenezo lazima wakurugenzi wa halmashauri watawajibishwa,"amesisitiza Mhe. Majaliwa.

Anasema kila Halmashauri lazima iweke mpango wa matengenezo wa magari hayo ili ziweze kufanya kazi kwa muda mrefu na kuweza kufamnya kazi iliyopangiwa ya kuhakikisha inafanya ufutiliaji wa elimu katika shule za msingi nchini.



Anafafanua kuwa magari hayo yatumike kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Halmashauri na kuhakikisha yanafuatilia ufundishaji na ujifunzaji wa elimu katika Wilaya ili malengo yaweze kufikika na kukamilika kwa wakati

Mh Majaliwa anatumia fursa hiyo kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuwachukulia hatua Maafisa Elimu wote ambao watayatumia magari hayo kinyume na kazi iliyopangiwa ya ufuatiliaji wa masuala ya elimu katika halmashauri kwa kuwa watakuwa wameenda kinyume na matakwa ya Serikali.

Hata hivyo, amewaagiza Maafisa Elimu wote nchini kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi kwa kuwa ndio msingi wa mafanikio



*Magari yaliyokabidhiwa kwa maafisa elimu wa halmashauri 184 yaliyonunuliwa kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R)*

kufuata sheria na taratibu za utumishi wa umma na imarisheni mahusiano katika utendaji kazi wa kila siku ili kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali ya kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Aidha ametaka maafisa elimu nchini kuwatumia madiwani katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto na kuhakkisha wazazi wanawajibika katika suala zima la kutimiza majukumu yake katika kuhakikisha watoto wanapata elimu



*Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akiwa na Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu (kushoto) wakikata utepe kuzindua magari ya maafisa elimu ya msingi yaliyokabidhiwa kwa halmashauri 184.*

katika maeneo yao kwa kuwa kiwango cha mafanikio ya elimu kilichofikiwa bado kinahitaji nguvu zaidi ili kufika mbali.

Amewataka kuhakikisha wanawatia moyo waalimu katika kutekeleza majukumu yao, watembeleeni, wasikilizeni na wahudumieni kwa bora.


Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Ummy Mwalimu anasema magari hayo yamenunuliwa na Serikali kupitia Programu ya EP4R kwa gharama ya Sh bilioni 16.4.



*Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge - Dodoma*



*Shule ya Msingi Mtemi Mazengo - Dodoma*



*Muonekano wa Shule ya Sekondari Lyamungo - mkoani Kilimanjaro baada ya ukarabati.*



*Shule mpya ya Elimu Jumuishi - Patandi Maalum, iijini Arusha*

# HALMASHAURI NNE KIKAANGONI UKUSANYAJI MAPATO




WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu amewataka Wakurugenzi wa Halmashauri za Longido, Same, Uvinza na Bumbuli kujitathmini katika suala zima la ukusanyaji wa mapato na kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo.

Waziri Ummy ameyasema hayo wakati akitoa taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato ya ndani ya Halmashauri katika kipindi cha Julai,2020 hadi Machi,2021 Jijini Dodoma.

Amesema Halmashauri zilizokusanya mapato chini ya asilimia 75 zinatakiwa kujitathmini na Halmashauri zijitathimini zaidi katika ukusanyaji mapato na upelekeaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo.

Amesema Halmashauri ya Longido kwa mara ya pili sasa anaingiza fedha ambazo si za mapato ya ndani kwenye mfumo wa mapato ili ionekane wamekusanya zaidi.

" Ingekuwa mara ya kwanza tungeweza kuvumilia lakini kwa mara ya pili sasa ameingiza fedha walizolipwa Fidia kutoa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwenye mfumo wa mapato takribani shilingi Mil. 700, hili hatuwezi kulivumilia tutachukua hatua," alisema Mhe.Ummy.

Ameongeza kuwa Halmashauri za Same, Bumbuli na Uvinza wanapaswa kujithathimini kwa Halmashauri zao kuchangia asilimia 4 tu ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/21.

" Halmashauri hizi hazifanyi vizuri kabisa mfano Same wamekusanya shilingi milioni 594 ila wametoa shilingi milioni 26 tu kwa ajili ya maendeleo sasa milioni26 zinafanya kazi gani ya kueleweka," amehoji Mhe.Ummy.

Aidha Mhe. Ummy amesema Halmashauri ya Uvinza kuwa imekusanya Sh milioni 624 na kwenye maendeleo wamepeleka Sh milioni 26 tu huku Bumbuli ikikusanya Sh milioni 336 na kupeleka Sh milioni 13 tu kwenye miradi ya maendeleo.

Taarifa ya mapato iliyotolewa na Mhe.Ummy inaainisha ufanisi wa kila halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kulinganisha makisio idhinishwa na mapato halisi.

Kwa kwaka wa fedha 2020/21, halmashauri zilipanga kukudanya Sh bilioni 814.9 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na katika kipindi cha Julai,2020 hadi Machi, 2021 Halmashauri zimekusanya jumla ya Sh bilioni 557.45 ambayo ni sawa na asilimia 68 ya makisio ya mwaka.

# BILIONI TATU ZANUNUA VIFAA VYA MAABARA




SERIKALI ya Awamu ya Sita inaendelea na azma ya kuboresha utoaji wa elimu nchini katika kuimarisha uchumi wa viwanda.

Hii ni katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka, 2014 ambayo pamoja na mambo mengine, imeweka malengo ya kuwa, na idadi ya kutosha ya wananchi walioelimika katika sayansi na teknolojia na kukidhi mahitaji ya maendeleo ya taifa. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefanya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia hususani kwa masomo ya sayansi na wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Serikali imenunua vifaa mbalimbali vya maabara kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika Shule za Sekondari vyenye jumla ya Sh 3,949, 98, 43.03.

Vifaa hivi vitagawanywa kwa shule za sekondari 1, 253 nchini na vitatumika katika maabara za Fizikia, Kemia, na Biolojia.

Huu ni utaratibu wa kawaida wa Serikali kuhakikisha kuwa, inaimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika shule za sekondari kwa lengo la kuhakikisha kuwa nchi inapata wataalam wa kada mbalimbali wenye maarifa ya kutosha katika kuchangia kuimarisha uchumi wa viwanda. Ni imani ya Serikali kuwa, vifaa hivyo vitatumika katika kuimarisha utoaji wa elimu kwa njia ya vitendo na kuandaa wanasayansi na wataalam bora ambao sio tu watachangia katika uzalishaji bali watatumika katika kutoa mchango wao nchini na nje ya mipaka ya nchi.

Niwatake walimu wa masomo hayo na wataalam wa maabara kwenye shule zote za sekondari za serikali kuhakikisha kuwa wanaweka utaratibu mzuri wa kutumia na kutunza vifaa vya maabara ili viweze kutumika kwa muda mrefu na kuwanufaisha wanafunzi wengi na kwa muda mrefu.



*Naibu waziri Mhe. David Silinde (Katikati) akikagua baadhi ya vifaa wakati wa uzinduzi wa ugawaji na usambazaji wa vifaa vya maabara kwa shule za sekondari na vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye uhitaji maalumu.*



# "MARUFUKU KUTUMIA TIKETI ZA BANDO"

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(OR-TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu, ameagiza kuanza kutumia tiketi za kielektroniki katika usafiri wa mabasi yaendayo kwa haraka kwa kutumia mfumo wa POSS kuanzia Julai Mosi, 2021, ili kudhibiti upotevu wa mapato.

Mhe. Ummy ameyasema hayo wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuhusu kuboreshwa kwa usafiri huo.

"Utekelezaji wa hilo ni hatua za awali wakati unasubiriwa mfumo mkubwa utakaohuisha matumizi ya kadi na mageti ambao ndio utakaokuwa ni suluhu ya kudumu,"amesema.

Ametaka uhakiki huo wa kutumia POSS kuanza haraka wakati mfumo mkubwa unaotarajiwa kutekelezwa Novemba mwaka huu, unasubiriwa ili kuepuka udanganyifu, wizi na upotevu wa mapato.

"Nataka mapema tuwe tumekomesha utoaji wa tiketi zisizohakikiwa, hapa tunaruhusu wizi kufanywa watu wanakuwa na vitabu vyao vya tiketi, Rais Samia na Waziri Mkuu waliyasema haya,"amesema.

Amebainisha matumizi ya tiketi hizo kunasababisha kujitokeza kwa udanganyifu na wizi wa mapato kutokana na baadhi ya watendaji wasio waaminifu kuingiza sokoni tiketi zao na kusisitiza kuwa lazima kuwepo kwa utaratibu unaohakikisha tiketi zinatolewa moja kwa moja katika mashine na kumfikia abiria wakati huo Waziri Ummy amesema mrundikano wa abiria katika vituo vya mwendokasi ni vyema ukapatiwa ufumbuzi kutokana kusababisha usumbufu kwa abiria na hivyo kupoteza malengo ya mazima ya uanzishwaji wa mradi huo ulioanza kutumika mwaka 2016 ukilenga kuondoa changamoto ya usafiri Dar es Salaam.

Aidha amewataka Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) kujidhatiti kwa kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuzidi kujiweka katika mazingira mazuri ya kupandishwa ya kupewa kazi ya kujenga mradi huo katika mikoa mingine ikiwemo ya Dodoma, Mwanza, Mbeya na Arusha.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa DART, Dkt. Edwin Mhede amesema malengo ni kuhakikisha wanatatua changamoto zote zilizopo sambamba na kubuni mikakati mipya ili kutimiza malengo ya taasisi hiyo iliyopewa jukumu la kutoa huduma za usafiri kwa wananchi

# ZIARA YA WAZIRI WA NCHI OR-TAMISEMI MIKOANI



**TANGA**

*Tanga Jiji, Mkinga na Muheza*

**DAR ES SALAAM**

*Manispaa ya Kinondoni*

**SHINYANGA**

*Shinyanga Manispaa na Kahama Mc*

**TABORA**

*Igunga na Tabora Manispaa*

**DODOMA**

*Chamwino, Bahi na Chemba*

## LENGO

- Kuzungumza  na Sekretarieti za Mikoa
- Kuzungumza na Kamati za Fedha za Halmashauri
- Kukagua Miradi ya Maendeleo




Hospitali ya Uhuru - Chamwino mkoani Dodoma



Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa

# MRADI WA DMDP SASA KUTEKELEZWA WILAYA ZOTE MKOA WA DAR ES SALAAM

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Ummy Mwalimu amesema Mradi wa Uboreshaji na Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP), utafanyika kwenye wilaya zote tano za mkoa huo, huku akitaka haki na usawa kutendeka katika mgawanyo wake.

Waziri Ummy amesema hayo wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa mradi wa DMDP awamu ya kwanza uliogharimu zaidi ya Sh bilioni 600, fedha zilizotolewa na Benki ya Dunia, ikishirikiana na Serikali.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, kwa sasa wanakamilisha majadiliano ndani ya Serikali kuhusu awamu ya pili ya mradi DMDP ambao mbali na kuboresha miundombinu ikiwemo barabara, mifereji pia unahusika na ujenzi wa masoko na sehemu za kupumzikia.

"Ofisa mratibu upo, mipango upo na rasirimali wa Tamisemi huu ndio ujumbe wangu lazima tuhakikishe kila manispaa inapata mgao, ingawa tutaangalia changamoto za kila manispaa lakini kila halmashauri lazima zipate kiuhalali.

" Siyo manispaa moja fedha nyingi au kilomita nyingi za barabara kuliko nyingine," amesema Waziri Ummy.

Kabla ya kueleza hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla alimweleza waziri Ummy kuwa baadhi ya maeneo ya hayatanufaika na awamu ya pili ya mradi huo akimtaka waziri kuliangalia suala hilo.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu akimsikiliza Mratibu wa Miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya TARURA, Mhandisi Humprey Kanyenye wakati akikagua maendeleo ya kazi za mradi huo jijini Dar es salaam.*

# Waziri Ummy aunda Tume ya Uchunguzi Soko la Kariakoo



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu akikagua vizimba vya kufanyia biashara, wakati alipotembelea Soko la Kariakoo kwa lengo la kujionea uendeshaji wa soko hilo, jijini Dar-es-salaam*

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu ameunda tume huru ya kuchunguza kero na malalamiko ya wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo na kutoa siku 14 kukamilika kwa uchunguzi huo. Katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi na kusikiliza changamoto za wafanyabiashara wa soko hilo, jijini Dar-es-Salaam

Waziri Ummy amesema baada ya kuwasikiliza wafanyabiashara hao amegundua kuwa lipo tatizo katika soko hilo na tatizo kubwa ni ukosefu wa mahusiano mazuri kati ya wafanyabiashara na menejimenti ya ya Shirika la masoko la Kariakoo, uwepo wa tuhuma za rushwa kwa baadhi ya viongozi wa soko, tozo kubwa la kodi na uwepo wa madalali wa vigoli pamoja na uwepo wa ubadhirifu wa fedha za mali za Shirika la Masoko ya Kariakoo. Ameiagiza Tume hiyo kuhakikisha inapitia kwa kina malalamiko yaliyowasilishwa na wafanyabiashara hao ili yaeze kupatiwa ufumbuzi na Serikali kwa wakati na kufanyiwa uamuzi utakaosaidia kulipeleka taifa mbele katika kuhakikisha wafanyabaishara wanafanya biashara zao katika mazingira mazuri kwa gharama zinazokubalika na Serikali.

Akizungumzia uwepo wa madalali Waziri Ummy amesema kuwa kuna wapo madalali waliojimilikisha vizimba na vigoli katika soko hilo ambapo wanawapingisha wafanyabiashara wadogo kwa gharama kubwa hali hii inarudisha nyuma juhudi za Serikali za kuhakikisha watu wake wanapata maeneo ya kufanyia biashara ili kujikwamua kimaisha na kujiongezea kkipato

Aidha, ameiagiza Tume huru ya uchunguzi kuishauri Serikali kama upo umuhimu wa kuendelea kuwepo kwa Shirika la Masoko ya kariakoo kwa kipindi cha wakati wa sasa kulingana na mabadiliko ya kisayansi na teknolojia



*Waziri wa Nchi, OR TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu akizungumza na wafanyabishara kujua changamoto zao mara baada ya kutembelea Soko la Kariakoo*

# Maelekezo ya jumla ya Waziri Ummy ziarani



Sekretariet za Mikoa zihakikishe zinasimamia na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mujukumu ya MSM ipasavyo.

Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinakusanya mapato ya ndani ipasavyo na zinafikia malengo waliojiwekea kwenye Bajeti ya 2020/21.

Pia halmashauri zote nchini kudhibiti matumizi ya fedha za mapato ya ndani na zile zinazoletwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Halmashauri zote kuhakikisha zinapeleka bajeti ya fedha za mapato ya ndani iliyotengwa kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi hiyo iwe ile inayolenga kutatua kero za wananchi.

Halmashauri zote nchini zote zihakikishe zinatoa asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mikopo ya Vijana, Wanawake na Walemavu na kufuatilia marejesho.

Viongozi na watumishi katika mikoa, wilaya na halmashauri zote kuhakikisha wanafanya kazi kama timu moja na kudumisha mahusiano mema baina yao.

Kuongeza usimamizi na ufuatiliaji kwenye miradi inayojengwa kwa kutumia "Force Account" ili kuhakikisha miradi hiyo inajengwa kwa ubora unaokusudiwa.

# PROF. SHEMDOE ATEGUA KITENDAWILI CHA UHAMISHO



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof,.Riziki Shemdoe akitoa ufafanuzi kuhusu uhamisho wa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa*

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe amesema uhamisho wa watumishi wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa utafanyika mara nne kwa mwaka yaani kila robo ya mwaka husika.

Akizungumza na waandishi wa habari Prof. Shemdoe amesema kila tarehe 10 ya mwezi unaofuata baada ya robo mwaka kwisha uhamisho utafanyika na majina yatawekwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

“Robo kwanza ya mwaka yaan Julai - Septemba majina ya uhamisho yatakua yanatoka tarehe 10 October, na robo ya Pili Oktoba - Desemba majina ya uhamisho yatatoka Januari 10.

“Katika robo ya tatu ya Januari-Machi majina ya uhamisho yatatoka April 10 na robo ya mwisho ya Aprili-Juni majina ya uhamisho yatatoka Julai 10,”amesema.

Aidha Prof.Shemdoe amebainisha kuwa majina ya watumishi wote watakaohamishwa yatawekwa kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz .

Pia amewataka Makatibu Tawala wa Mikoa yote nchini kuwasilisha orodha ya watumishi wa kuhama ofisi ya Rais-TAMISEMI kila tarehe 05 ya mwezi unaofuata baada ya robo mwaka.

Aidha, amesisitiza Makatibu Tawala wote kutokupitisha maombi ya watumishi wanaotaka kuhamia kwenye majiji, manispaa na miji kwa kuwa maeneo hayo yana idadi kubwa ya watumishi.

Aidha, Prof.Shemdoe amewataka Makatibu Tawala kuwapa kipaumbele watumishi wenye changamoto mbalimbali zilizothibitishwa.

Pia amehimiza watumishi wote kubaki kwenye vituo vyao na barua za uhamisho zitatumwa kwa waajiri wao na wataona majina yao kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Pia amewaasa watumishi kujihadhari na matapeli wanaotaka fedha kwa ajili ya kufanikisha uhamisho wao kwa kuwa uhamisho ni bure na ni haki ya kila mtumishi.

Amesema kuwa barua za uhamisho za kipindi cha nyuma ambazo zilishafika Ofisi ya Rasi TAMISEMI zinashughulikiwa na majina yatatolewa kila mwezi mpaka Juni 30 kabla utaratibu mpya haujaanza kutumika

## NAIBU WAZIRI DUGANGE AKIWA ZIARA KWENYE MIKOA NA HALMASHAURI NCHINI

“Viongozi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hakikisheni mnasimamia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi ya afya ili iweze kukamilika kwa wakati na wananchi wapate huduma.”

“Waganga wakuu wa mikoa na wilaya simamieni uwekaji kumbukumbu kwenye vituo vya kutolea huduma hasa kwenye maeneo ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi vinavyonunuliwa pamoja na mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa.”

“Waganga wakuu wa mikoa na wilaya simamieni ukusanyaji wa mapato kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili vituo hivyo viweze kujiendesha na kuacha utegemezi kwenye ruzuku ya Serikali.”

“Waganga wakuu wa mikoa na wilaya wekeni mifumo mizuri ya utambuzi wa wananchi wanaostahi kupata msamaha wa matibabu.”

“Waganga wakuu wa mikoa na wilaya hakikisheni mnasimamia nidhamu na maadili ya watumishi katika sekta ya afya.”

# WASICHANA WOTE WENYE SIFA WACHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO, VYUO - 2021




*Mhe. Ummy Mwalimu,*
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Ummy Mwalimu amesema wanafunzi 148,127 wachaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi.

Aidha, wasichana wote waliokidhi vigezo na kupata daraja la kwanza hadi la tatu wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi kwa mwaka 2021.

Akitoa taarifa ya uchaguzi huo kwa waandishi wa habari Jijini Dodoma, wasichana 63,878 na wavulana 84,249 sawa na asilimia 33.84 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2021.

Waziri Ummy amesema kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha inawainua wanawake ambapo kwa mwaka huu wanafunzi wasichana wote waliokidhi vigezo na kufaulu mitihani yao wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ameendelea kufafanua kuwa wanafunzi 87,663 wakiwemo wasichana 41,885 na wavulana 45,778 sawa na asilimia 59.18 ya wenye sifa wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule 476 za Serikali zikiwemo shule mpya 42, wanafunzi wenye mahitaji maalum 288 sawa na asilimi 100 walikuwa na sifa ya kujiunga na kidato cha tano.

Vilevile, wanafunzi 41, 504 wakiwemo wasichana 17,646 na wavulana 23,858 sawa na asilimia 47.34 wamechaguliwa kujiunga na masomo ya tahasusi za Sayansi na Hisabati na wanafunzi 46,159 wakiwemo wasichana 24,239 na wavulana 21,920 sawa na asilimia 52.66 wamechaguliwa kujiunga na tahasusi za masomo ya sanaa na biashara.

Amesema wanafunzi 1598 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam , Chuo cha Usimamizi wa Maendeleo ya Maji na Chuo cha Sanyansi na Teknolojia Mbeya.

Waziri Ummy amebainisha idadi ya wanafunzi wenye sifa za kuchaguliwa kujiunga na kidato cha Tano na vyuo vya elimu ya ufundi imeongezeka kwa asilimia 14.07 kutoka 129,854 mwaka 2020 hadi 148,127 mwaka 2021 ikiwemo wasichana 63,878 ambao wamechaguliwa wote.

Amesema kuwa idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano kwenye tahasusi za Sayansi na Hisabati imeongezeka kwa asilimia 14.10 kutoka 36,375 mwaka 2021 hadi kufikia 41,504 mwaka 2021 wakiwemo wasichana 17,646.

Vile vile, amesema kuwa idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na vyuo vya Ualimu (Stashahada na Astashahada) imeongezeka kwa asilimia 28.44 kutoka 5,813 mwaka 2020 hadi 7,466 mwaka 2021 ikiwemo wasichana 3,235.

# WAKURUGENZI ACHENI KUBANA FEDHA ZA LISHE - PROF. SHEMDOE



*Prof. Riziki Shemdoe*
*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI.*

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuhakikisha fedha zinazotengwa katika bajeti kwa ajili ya shughuli za afua za lishe zinatolewa ili kutokwamisha kazi hizo.

Akifungua kikao cha siku tatu tarehe 28 Aprili, 2021, jijini Dodoma, Prof. Shemdoe amesema kila mwaka serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kushughulikia masuala ya afua za lishe, lakini tatizo hutokea wakati wa upangaji wa vipaumbele.

Amesema licha ya ongezeko la bajeti katika mamlaka za serikali za mitaa kutoka Sh bilioni 11.6 kwa mwaka 2017/18 hadi Sh bilioni 16.87 kwa 2019/20 lakini kumekuwa na utoaji wa fedha za afua za lishe usio wa kuridhisha.

"Kuanzia sasa pamoja na vipimo vingine vya ufanisi vinavyotumika kuwapima wakurugenzi, suala la afua za lishe kitakuwa ni kigezo muhimu katika kuwapima watendaji hao, hivyo lazima wahakikishe masula yote ya suala la lishe yanapewa kipaumbele" amesema Prof. Shemdoe.

Pia, Katibu Mkuu amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuzingatia miongozo inayotaka kutengwa Sh 1,000 kwa kila mtoto aliye chini ya miaka mitano kwa ajili ya lishe.

Awali, Mratibu wa Lishe, TAMISEMI, Mwita Waibe amesema tangu kuanzisha idara katika mamlaka za serikali za mitaa pamoja na mambo mengine wameanzisha mfumo wa (Information Management Monotoring and Evaluation System -IMES), ambao unafuatilia na kupata takwimu sahihi za afua za lishe.

Mwita amesema sekta ya lishe ina changamoto ya watumishi kwani katika mikoa 26 ni mikoa 20 tu yenye wataalamu wa lishe na kati ya halmashauri 184 ni halmashauri 66 pekee zenye wataalamu hao.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki 80 wa mkutano huo, Mwenyekiti wa Maofisa Lishe nchini, Bi.Bertha Donald ameiomba serikali kuhimiza utoaji wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya lishe katika halmashauri.

# WAZIRI UMMY NA VIKAO VYA IDARA



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu akiwa katika Kikao na watumishi wa moja ya Idara za Ofisi ya Rais - TAMISEMI,-- Jijini Dodoma.*

## Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe:

Kwa pamoja na Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) walifanya mapitio ya kazi zilizotekelezwa, vipaumbele pamoja na kuweka mikakati ya kuboresha huduma za afya ya msingi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri

## Idara ya Usimamizi wa Elimu:

Kwa pamoja na Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) walifanya mapitio ya kazi zilizotekelezwa, vipaumbele vya Idara hiyo na kuweka mikakati ya kuboresha upatikanaji wa elimu kuanzia ngazi ya awali msingi na sekondari.

## Idara ya Maendeleo ya Miundombinu:

Kwa pamoja na wataalamu waliweka mikakati ya pamoja na kuboresha ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini.

## Idara ya Uendelezaji Miji na Vijiji:

Mhe. Ummy alisisitiza umuhimu wa kuweka na kutekeleza mikakati mahususi ya kupanga, kuendeleza na kurembesha miji na vijiji ikiwemo kutumia mfumo wa GIS na Mpango Maalum wa kuendeleza Miji Midogo inayochipukia.

# WAZIRI UMMY AKOSHWA NA UTENDAJI WA WATUMISHI TAMISEMI



WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu, ameridhishwa na kiwango cha utendaji kazi cha watumishi wa ofisi hiyo kwakujitoa na kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake bila kutegea.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo, amesema pamoja na muda mfupi alionao katika Wizara, lakini amekoshwa na kiwango cha utendajikazi, kwakuwa watumishi wa TAMISEMI wamekuwa wakijitoa kwa muda wa ziada ili kukamilisha malengo waliyojiwekea.

“Nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kazi nzuri zilizofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na kukamilisha Jengo la Ofisi katika Mji wa Serikali wa Magufuli (Magufuli City) Mtumba na kuhamia, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Ujenzi wa Majengo ya Utawala katika Mikoa, Halmashauri, Tarafa, Kata, Mitaa na Vijiji,” amesema Mhe. Ummy.

Waziri Ummy amesema, Ofsi ya Rais-TAMISEMI, imefanya kazi kubwa ya usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kusimamia na kufanikisha uandikishaji wa wanafunzi wa Darasa la Kwanza kutokana na Sera ya Elimu bila malipo lakini pia amepongeza kwa usimamizi imara ulio wezesha kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita.

“Natambua kumekuwa na ongezeko la mapato ya ndani katika ngazi ya halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali kama vile, ushuru wa mazao, ushuru wa huduma, vibali, ushuru wa magulio na masoko, ada za shule kwa Kidato cha Tano na Sita na ada za uchangiaji huduma za afya na vyanzo vinginevyo kulingana na mapato lindwa ya halmashauri husika, hii yote ni kazi yakupigwa mfano ambayo TAMISEMI mmeweza kusimamia ikiwepo ujenzi wa madarasa, maabara, mabwalo na mabweni katika shule zetu,” amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema mabaraza ya wafanyakazi yapo kisheria hivyo yatumike katika kujadili kwa kina mambo yote waliyopanga ili tija iliyo kusudiwa ipatikane.

Awali, akimkaribisha kwa ajili ya uzinduzi wa Baraza hilo, Mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, amesema madhumuni ya Baraza la Wafanyakazi ni kutoa fursa kwa watumishi kupitia wawakilishi wao, kujadiliana juu ya masuala mbalimbali ya msingi yanayohusu tija na ufanisi kwa upande mmoja na maslahi ya watumishi kwa upande mwingine.

“Baraza la Wafanyakazi linaongeza ushiriki wa wafanyakazi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi yao kama ilivyofanuliwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105,” alisema Prof. Shemdoe.

Kupitia kikao hicho, wajumbe wa baraza hilo la wafanyakazi, limepitisha kwa kauli moja bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI yenye jumla ya Sh 7,683,329,644,800 kwa ajili ya Fungu Na.56 Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Fungu no. 2. Tume ya Utumishi wa Walimu na Mafungu 26 ya Mikoa.

# SERIKALI YAAJIRI WATUMISHI 2,946 KWA KUSHIRIKIANA NA MKAPA FOUNDATION



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI (afya) Dkt. Grace Magembe akitoa taarifa ya ajira za watumishi 2,946 zilizotolewa na Serikali kwa kushirikiana na Benjamin Mkapa Foundation

SERIKALI kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa, chini ya ufadhili wa wadau wa maendeleo hapa nchini, wamefanikiwa kuajiri watumishi wapya wa afya kwa kada mbalimbali 960 na watoa huduma za Afya Ngazi ya Jamii 1986 kwa mikataba ya kuanzia mwaka mmoja nakuendelea.

Akizungumza na vyombo vya habari, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Afya, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Dkt. Grace Magembe kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mhe. Ummy Mwalimu amebainisha mchango huonwa wadau katika sekta ya Afya kwa kuwezesha upatikanaji wa Ajira za watumishi wa Afya ngazi ya Serikali za Mitaa.

Amesema ajra hizi zimezotolewa kwa mikataba ya kuanzia mwaka mmoja na kuendelea, ni tofauti na ajira 2720 za sekta ya Afya zilizotangazwa hivi karibuni kupitia agizo la Rais wa Jamuhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.
Dkt. Grace ameeleza kuwa Watumishi hao wameajiriwa kutoka
katika kanzidata ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikiwa ni waombaji wenye sifa wa ajira za afya zilizotangazwa kipindi cha nyuma lakin hawakuweza kuajiriwa wote kutokana na ufinyu wa nafasi hizo.

"Upatikanaji wa watumishi hawa ni sehemu ya mipango ya Serikali kwa kushirikiana na wadau kuweka mifumo imara ya utoaji huduma za afya kwa watanzania wote,"amesema
Amebainisha idadi hiyo ya watumishi imekuja wakati muafaka ambapo Serikali inatekeleza vipaumbele vyake hususani katika kuhakikisha utoaji huduma bora katika kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza na sambamba na kuongeza nguvu ya kupambana na magonjwa ya mlipuko kama vile maambukizi ya Homa kali ya Mapafu (UVIKO- 19).

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Benjamini Mkapa Dkt. Ellen Mkondya-Senkoro, amesema wadau waliowezesha kuajiriwa kwa watumishi hao ni Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund), Shirika la UNICEF, Irish Aid na Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO) ambao wameipatia Tanzania fedha kupitia Taasisi ya Benjamin William Mkapa ili iweze kuajiri watumishi hao.

Dkt. Ellen ameongeza kuwa kiasi cha fedha zitakazotumika wakati wote wa ajira za watumishi hao kwa kulipa mishahara na stahiki zingine ni Sh bilioni 19.

Ajira hizi zimekuja wakati muafaka ambapo Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI imejenga Hospitali za Wilaya 102, Vituo vya Afya 488 Zahanati 1198 na nyumba za watumishi 840 vituo vyote hivi vinahitaji watumishi wenye ujuzi na na weledi ili kuweza kutoa huduma bora.



Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ustawi wa Jamii Rashid Maftaha (kulia) na Dkt. Ellen Mkondya-Senkoro Mtendaji Mkuu wa Benjamin Mkapa Foundation

# PROF. SHEMDOE ATAKA TATHMINI UJENZI WA BARABARA ZA MJI WA SERIKALI



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe akisisitiza jambo wakati akikagua mradi wa ujenzi wa barabara za Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.*

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe ameagiza ifanyike tathmini ya kina ya muda wa nyongeza ulioombwa na mkandarasi wa barabara za Mji wa Serikali Mtumba zinazojengwa kiwango cha lami.

Mradi huo kwasasa ujenzi wake umefika asilimia 70 na unatakiwa kukamilika mwezi ujao lakini mkandarasi kutoka Kampuni ya China Heinan International Cooperation Co.Ltd (CHICO), ameomba nyongeza ya miezi 10 ili kukamilisha asilimia 30 iliyobaki.

Akizungumza mara baada ya kukagua ujenzi huo, Prof. Shemdoe amesema mradi huo ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 18 ambapo kwa mujibu wa mkataba ni Julai 31, 2021.

"Kazi imefanyika tumeiona na kiwango kilichofikia ni asilimia 70, gharama ya mradi huu ni Sh bilioni 89.1 na barabara zinazojengwa jumla ni kilometa 51.2 kazi iliyofanyika ni kubwa, tunajua hadi Julai 31, 2021 hii kazi ya asilimia 30 iliyobaki itakuwa bado haijakamilika."

"Mkandarasi kuomba nyongeza ya muda ya miezi 10 hili ombi sijaliafiki nimemuagiza mkandarasi mshauri wa mradi huu kwamba pamoja na maombi hayo afanye tathmini ya kina ya maombi hayo lakini mimi sijaafiki."

"Hiyo miezi ni mingi iliyoombwa kama mradi huu umetumia miezi 16 kujenga kwa asilimia 70 sioni sababu ya mkandarasi atumie miezi 10 kukamilisha asilimia 30 iliyobaki, namuelekeza mshauri kwa kushirikiana na TARURA na Meneja wa Mradi wahakikishe wanafanya tathmini ya kina ya muda ulioombwa ili kupata muda muafaka na kazi iishe mapema,"amesema.

Pia ameagiza kuangalia namna ya kuhusisha suala la upandaji miti kwenye barabara hizo, na pia vijengwe vibanda vya abiria kwa ajili ya kusubiri usafiri.

Aidha, amewahakikishia kuwa hati za malipo zote zilizowasilishwa za Sh bilioni 44 kwa mkandarasi zote zimelipwa.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Samia Suluhu Hassan alihakikisha madeni yote yaliyokuwa yamebaki yamelipwa, na tumezilipa na mimi nimesaini malipo yale, mkandrasi asije kulalamika anaidai serikali haidai serikali mshauri naye alikuwa anadai Sh milioni 700 zote tumemlipa kwa hiyo asije kusema anashindwa kusimamia kazi hii kwa kisingizio cha kudai fedha, tunataka kazi hii ikamilike kwa wakati,"amesema.



*Barabara zinazoendelea kujengwa mji wa Serikali Mtumba - Dodoma*



# WAFANYAKAZI WA OFISI YA RAIS – TAMISEMI WAADHIMISHA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI




WAFANYAKAZI wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wameadhimisha siku ya wafanyakazi duniani kwa kushiriki maandamano na sherehe za kimkoa zilizofanyika kwenye uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma.

Wakiwa uwanjani hapo 01.05.2021, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye kwasasa ni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dkt. Binilith Mahenge, amesema Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya wafanyakazi kwa kusikiliza na kufanyia kazi kero zote zinazowakabili na nyingine kuzipeleka sehemu husika kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi kwa maslahi ya wafanyakaz wote.

Dkt. Mahenge amesema kuwa, zipo changamoto ambazo zinaweza kushughulikiwa kwa ngazi za chini ambapo wapo watu waliopewa mamlaka wanaweza kuzitatua na hivyo sio lazima mpaka ziende ngazi za juu, miongoni mwa changamoto hizo ni kucheleweshwa kwa kupata mafao kwa mtu aliyestaafu amesema, kero hizo zinapaswa kufanyiwa maandalizi mapema kupitia kwenye mamlaka zetu tunazosimamia sio mpaka mpaka mtu anastaafu ndio aanze shughulikiwa.
“Kwa mtu aliyestaafu anapoanza kufuatilia mafao yake anasumbuliwa mpaka anachukia serikali yake na hiyo ni kutokana na baadhi ya watumishi kutotekeleza majukumu yao ipasavyo,” amesema Dkt. Mahenge.

Dkt. Mahenge ametoa rai kwa wizara na taasisi kuwaruhusu watumishi kujiunga na vyama vya wafanyakazi kwa maslahi ya kuweza kuwasemea kero zao.




*Watumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakiwa kwenye maandamano wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani*

# MAPOKEZI YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS - TAMISEMI



*Katibu Mkuu, Prof. Riziki Shemdoe akikabidhiwa ua mara baada ya kuwasili Ofisi za TAMISEMI tayari kuanza majukumu yake mara baada ya kuapishwa*

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, amewataka watumishi kuwa na mshikamano ili kuweza kutimiza azma ya Serikali yakuwaletea wananchi Maendeleo.

Prof. Shemdoe ametoa Kauli hiyo wakati alipowasili katika Ofisi zilizopo eneo la Mtumba jijini Dodoma. "Ninyi watumishi asilimia kubwa ya muda wenu mnautumia mkiwa kazini, hivyo fanyeni eneo la kazi kuwa sehemu salama, yenye amani na upendo wakati wote," amesema.

Prof. Shemdoe ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI akichukua nafasi ya Mhandisi Joseph Nyamhanga.




*Aliyekuwa Katibu Mkuu, OR Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga akimkabidhi ofisi Prof. Riziki Shemdoe mara baada ya kuteuliwa na kuapishwa kushika wadhfa huo.*

# MAJALIWA AAGIZA SOMO LA MICHEZO KUFUNDISHWA KUANZIA SHULE YA AWALI




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akikabidhi mpira wakati akifungua mashindano ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara*

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) ameelekeza ufundishaji wa somo la Michezo uimarishwe kuanzia shule ya awali, msingi, sekondari na vyuo ili kujenga hali ya kujiamini na kuwa mahiri kimwili na kiakili.

Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa ameyasema hayo leo wakati akifungua mashindano ya michezo na taaluma yajulikanayo kama UMISSETA na UMITASHUMTA yaliyofanyika kwenye uwanja wa Nangwanda Sijaona Mkoani Mtwara.

Ameeleza michezo ni muhimu zaidi kwa makuzi na maendeleo ya taaluma ya watoto na vijana na ina mchango mkubwa katika kuimarisha afya ya mwili na akili.

"Watafiti wamethibitisha kuwa michezo kwa madarasa ya awali kwa maana ya miaka 3-6 ni muhimu zaidi katika kuongeza uwezo wa mzunguko wa damu katika ubongo (kuongezeka kwa mishipa ya damu) na maendeleo ya afya na makuzi ya watoto kwa ujumla wake hivyo ni vyema tukajikita kumjenga mtoto huyu kuanzia kwenye ngazi ya awali,"amesema Waziri Mkuu Majaliwa.

Ameongeza: "bila shaka sote tunaelewa kuwa binadamu hawezi kuwa na akili bora kwenye mwili dhaifu na afya bora inaweza kujengwa vizuri zaidi kwa kushiriki katika michezo hivyo tujikite katika kutengeneza vizazi vitavyokua na mahiri kwenye michezo wakati wote maisha yao."

Majaliwa alibainisha kuwa katika siku za hivi za karibuni kumekuwepo na mafanikio makubwa ya vijana waliyoyapata kupitia Michezo na wengi ni wa hapa hapa Tanzania, kama vile Mbwana Samata.

"Kwa hawa wachache wanatuonyesha picha kubwa ya namna ambavyo vijana wetu wengi wanaweza kufanikiwa kupitia michezo na sanaa tuongeze nguvu katika eneo hili," amesema.

Aidha amesema Michezo na Sanaa vikiwekewa mipango sahihi vina nafasi kubwa ya kuchangia na kujenga uchumi endelevu wa Taifa na watu wake.

"Sekta hizi ni fursa kubwa kwa vijana wetu kujiajiri, kuajirika na

*inaendelea uk. 38*

inatoka uk. 37

# ...ili kuwajengea ujuzi, maarifa, umoja na uzalendo



kuutambulisha utamaduni wetu ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu,"amesema.

Amewataka wanafunzi wote wanaoshiriki katika mashindano hayo kutokuridhika na hatua waliyofikia kwenye mashindano hayo na yawe mwanzo wa kujiimarisha katika michezo na sanaa ili kulitangaza taifa kupitia michezo na sanaa.

" Matarajio ya wengi ni kuona mkionyesha uwezo wenu kwa nidhamu ya hali ya juu na kuiletea mafanikio mikoa yenu na taifa kwa jumla,"amesema.

Amezitaka Wizara zinazohusika kurudisha mafunzo ya michezo katika vyuo vya Butimba na Mtwara ili kufundisha walimu watakaoweza kuwapa wanafunzi mafunzo sahihi ya michezo.

Kwa upande wake, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Innocent Bashungwa amesema wanakusudia kuanzisha vituo vya kulea vipaji katika shule mbalimbali ili kuhakikisha kuwa vipaji vya watoto vinaendelezwa kuanzia umri mdogo.

Naye, Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mhe. Davidi Silinde ameelezea malengo ya mashindano hayo kuwa ni kujenga umoja wa kitaifa, mshikamano na upendo baina ya wanafunzi wangali katika umri mdogo.

Amesema pia kuimarisha Taaluma ya Michezo kwa wanafunzi ili kuwajengea ujuzi na maarifa na kuwa mahiri wanapoendelea kukua pamoja na kujenga umoja, uzalendo na mshikamano miongoni mwa wanafunzi, walimu na wadau wa michezo nchini.

Pia ameongeza kuwa mashindano hayo yatawajengea watoto Ukakamavu na umahiri katika michezo pamoja na kuibua na kuendeleza vipaji vya wanafunzi wangali bado wachanga na kujenga dhana ya uvumilivu na ustahimilivu.

Mashindano hayo yamebeba kauli mbiu ya Michezo, Sanaa na Taaluma kwa maendeleo ya viwanda na jumla ya wanamichezo 3600 kutoka mikoa 26 watashiriki kwenye michezo ya UMITASHUMTA na wanamichezo 3800 kutoka katika mikoa 28 ya Tanzania Bara na visiwani.

Toleo na. 1

JUNE 2021

# TAMISEMI KAZINI



**JE** Una shida yoyote ya **kiofisi** na unahitaji kuhudumiwa?

Piga **simu**, tuma **ujumbe** mfupi na **whatsapp**

**+255735 160 210**

**+255262 160 210**

**KARIBU**
**TUKUHUDUMIE**

*www.tamisemi.go.tz*